*Kiswahili, Juz. 88 (1), 2025, 111-131*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Lugha ya Ungonoshaji katika Ushairi wa Bongo Fleva: Mifano kutoka Nyimbo Teule

*Winne Stephen Mtega*[1]

**Ikisiri**

Matumizi ya lugha inayoashiria ungonoshaji yamekuwa yakijitokeza katika nyanja mbalimbali katika jamii zote duniani. Ungonoshaji hujitokeza katika siasa, hotuba, nyimbo hususani katika lugha inayotumika na mazungumzo ya kawaida ya wanajamii (Ngunguti na Mapunda, 2021). Baadhi ya maneno yaliyongonoshwa yanapotumika, wasikilizaji huacha maana ya msingi kwa kupigia chapuo maana ya ziada ya neno husika ambayo mara nyingi huhusishwa na masuala ya ngono. Baadhi ya wataalamu wanalitazama suala la ungonoshaji katika Bongo Fleva kwa namna hasi kwamba ni ukengeushi wa misingi ya maadili ya Mwafrika, jambo ambalo linainyima jamii uhuru wa kujieleza (Ayisi, 1962; Van Pelt, 1971; Karama, 2019; Wanjala, 2020). Makala hii imefafanua matumizi ya lugha ya ungonoshaji katika ushairi wa Bongo Fleva na mifano imetoka katika wimbo wa "Kwangwaru" wa Harmonize na Diamond Platinumz (2018) pamoja na "Baikoko" wa Mbosso na Daimond Platinumz (2020). Data za makala zimepatikana kwa kutumia mbinu ya usikilizaji na utazamaji za nyimbo teule kutoka katika mtandao wa *YouTube*. Uchambuzi wa data umezingatia mkabala wa kitaamuli na kuongozwa na Nadharia ya Moduli Anuwai. Matokeo yanaonesha kuwa matumizi ya lugha ya ungonoshaji yana dhima ya kufanikisha mawasiliano, kubainisha umuhimu wa mafunzo ya jando na unyago katika jamii na kuonesha ubunifu wa kiutunzi.

## 1.0 Utangulizi

Kabla ya ujio wa wakoloni katika jamii za Kiafrika, masuala yanayohusishwa na ngono yalichukuliwa katika mtazamo chanya kwa kufungamanishwa na falsafa ya Kiafrika hususani masuala ya uzazi kama nyenzo ya kuiendeleza jamii. Pia, yalifungamanishwa na shughuli za kiuchumi na kitamaduni (Okechi, 2018; Karama, 2019; Bamgbose, 2001). Sanaa za maonesho mbalimbali zilizohusiana na masuala ya ngono zilifanyika katika maeneo ya wazi na zilihusisha sherehe za kijadi, ngoma na nyimbo (Matic, 2024). Katika shughuli hizo, ngono hazikutazamwa kama udhalilishaji au uvunjifu wa maadili bali ziliendeshwa kwa heshima ili kuonesha mshikamano wa kijamii na kitamaduni na kama njia ya kutunza na kuhifadhi falsafa ya jamii husika (Matić, 2024). Katika maonesho hayo, ngono haikufanyika hadharani

[1] Mhadhiri, Idara ya Lugha na Fasihi, Kitivo cha Insia na Sayansi za Jamii, Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Iringa, Tanzania.
Baruapepe: Winne.mtega@muce.ac.tz / Mtegawinnie19@gmail.com

bali ilipewa heshima kwa kuwekewa kanuni na taratibu maalumu zilizodhibiti maadili ya jamii. Baada ya ujio wa wakoloni, mtazamo wa kijadi kuhusu ngono ulibadilika. Karugendo (2020) anaeleza kuwa dini za Uislamu na Ukristo zilifanya ngono iogopwe na ionekane kama uovu. Kuanzia hapo, sheria za kidini na baadaye za kiserikali, zikawekwa ili kudhibiti mwenendo wa ngono katika shughuli za kijamii na sanaa. Ngono ikachukuliwa kama suala la siri na linalohusu wanandoa pekee. Hivyo, kusema hadharani masuala yanayohusu ngono ikawa kinyume na sheria (Van Pelt, 1971; Wanjala, 2020; Goodness, 2024). Mwelekeo huu unadumu mpaka sasa katika tamaduni za jamii mbalimbali nchini Tanzania. Kwa hiyo, makala hii inajiegemeza katika mwelekeo huu. Lengo lilikuwa kuchunguza dhima za matumizi ya lugha ya ungonoshaji katika ushairi wa Bongo Fleva.

Ungonoshaji ni neno lililonyumbuliwa kutokana na dhana ya ‘ngono’ inayomaanisha kitendo cha kujamiiana baina ya mwanamke na mwanamume (BAKITA, 2022; Lucas, 2022). Kwa mujibu wa Ngunguti na Mapunda (2021), ungonoshaji ni tabia ya kuyapatia tafsiri ya kingono maneno ambayo hayahusiani moja kwa moja na ngono. Anaongeza kuwa, wanajamii hususani watumiaji wa lugha ya Kiswahili wamekuwa wakiibua maana za maneno mbalimbali yanayotumika katika lugha hiyo na kuyafungamanisha kimaana na masuala ya kingono; iwe kwa misingi ya viungo vya ngono, mitindo ya ngono au tendo la ngono. Mara nyingi maana hizo huonekana kuwa ni za ziada kwa sababu huibuliwa na wasikilizaji. Fasili hiyo inaonesha kuwa fikra za wanajamii ndizo zilizobeba maarifa ya kingono, hivyo, hutumia fikra zao kutafsiri maneno kwa kuyahusisha na michakato ya kingono. Kwa mujibu wa Newman (2015), Deignan (2016) na Da Costa (2016), uhamishaji wa maana ni mabadiliko ya maana ya maneno kulingana na wakati. Uhamishaji huhusisha ukubwaishaji, udogoishaji, ubadilishaji, ubayaishaji, sitiari na metonimia (Traugott, 2006). Mchakato huu si wa kinasibu bali huchochewa na wasikilizaji kuhitaji kuelezea dhana mpya, kufafanua msamiati na istilahi mpya za kiteknolojia kulingana na mabadiliko ya kijamii. Anatoa mfano wa neno *gay* katika lugha ya Kiingereza lenye maana ya ‘mwangaza’, ‘furaha’, ‘uwezo wa kiakili’ kwamba kwa sasa limehamishwa kimaana na kutumika kuelezea mwelekeo wa kijinsia (Brown, 2015). Mfano huu unaonesha namna uhamishaji wa maana unavyoakisi mabadiliko makubwa ya kijamii ambayo yametoka katika maana ya msingi ya neno husika hadi ile ya ziada inayofungamanishwa na masuala ya ngono na kijinsia.

Aidha, Fortson IV (2003) anaeleza kuwa uhamishaji maana kutoka maana ya msingi hadi ya ziada hujitokeza kwa namna mbili. Kwanza, ni pale mzungumzaji anapotumia lugha ya picha kuwasilisha jambo aliloshidwa kuliwasilisha kwa namna ya kawaida. Pili, ni msikilizaji anapohusianisha kilichowasilishwa na mzungumzaji na maarifa aliyonayo huku akifungamanisha na tamaduni, muktadha wa uwasilishaji pamoja na uzoefu wa kimazingira. Mambo haya huchochea kuhamishwa kwa maana kutoka ya msingi kwenda ya ziada. Fortson IV anaongeza kuwa matumizi lugha za kisanaa hukusudia kutengeneza picha fulani na kuihusianisha na jambo au kitu kingine kimwonekano na kitabia ili kuleta athari katika fikra za msikilizaji, msomaji

au mtazamaji. Athari hizo huvuka mipaka ya kifasihi. Kwa maana hiyo, matumizi ya lugha kama sitiari, taswira, taashira na tafsida huchochea uhamishaji wa maana na uzalikaji wa maana mpya. Uhamishaji maana huonesha namna lugha inavyopokea mabadiliko kulingana na mabadiliko ya jamii (Deignan, 2016). Maana yake ni kwamba baadhi ya matumizi ya lugha za kisanaa kwa kiasi fulani ambayo hutumiwa na watunzi wa nyimbo za Bongo Fleva huashiria dhana ya ngono. Uashiriaji huo pia ndio unaoathiri wasikilizaji na kuchochea kuhamisha maana ya kilichowasilishwa katika nyimbo hizo kutoka ile ya msingi hadi ya ziada inayohusishwa na masuala ya ngono.

Kutokana na maelezo hayo, katika makala hii ungonoshaji unafasiliwa kama ni hali au tabia iliyojengeka katika fikra za wazungumzaji na wasikilizaji ya kuzungumza, kutafsiri, kuyapa maana na kuhusianisha na mchakato wa kingono maneno ambayo hayahusiani moja kwa moja na ngono. Utoaji wa maana hizo za ziada hujitokeza sana pale nyimbo za kizazi kipya zinapoimbwa. Uhusianishaji huo ndio tunaoutazama kama ungonoshaji. Nyimbo za Bongo Fleva ni utanzu wa ushairi simulizi ambao ulianza miaka ya 1980 nchini Tanzania. Bongo Fleva hujumuisha aina mbalimbali za nyimbo kama vile *Hip hop, RnB, Raga, Rhumba, Zuku na Rap,* taarabu na ngoma za asili (Suriano, 2006; Omari, 2009; Mahenge, 2010; Samwel, 2012). Historia ya nyimbo za kizazi kipya ilianza kushika kasi hapa Afrika Mashariki, hasa Tanzania katika miaka ya 1980. Vijana wengi katika Afrika Mashariki walitumia muziki wa kizazi kipya kueleza matatizo yanayowakumba kwa ujumla kama vile ukosefu wa ajira na ubaguzi wa kiuchumi, kisiasa na kijamii (Lupokela na Msuya, 2010; Bulaya, 2010). Muziki huu umebeba umaarufu mkubwa ndani na nje ya bara la Afrika ijapokuwa wengine wanauita kwa kejeli kama muziki wa ‘Kufokafoka’ (Samwel, 2012). Katika makala hii, majina ‘Bongo Fleva’, ‘Muziki wa Kizazi Kipya’ na ‘nyimbo za Bongo Fleva’ yametumika kama visawe.

Pamoja na nyimbo hizo kukubalika katika jamii, baadhi ya wataalamu na wadau wa Bongo Fleva wanaonesha kuwa zinakabiliwa na changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni za kimaadili, mavazi yasiyofaa, maudhui yaliyokengeuka, utendaji ambao huhusisha minenguo na miondoko inayokinzana na maadili ya Kiafrika pamoja na matumizi ya lugha ya kingono ambayo yanakinzana na maadili ya Mwafrika (Tupokigwe, 2010; Kadallah, 2010; Samwel, 2012; Jilala, 2015).

Matumizi ya maneno yanayoashiria ngono yameibua mitazamo hasi baina ya wanajamii, wanataaluma na baraza linalohusika katika kukagua ubora wa sanaa hizo kama vile BASATA[2]. Kwa mfano, Chachage (2002), Suriano (2006), Perullo (2007), Omari (2009), Samwel (2012) na Kasiga (2023), wanaeleza kwamba wanataaluma, wanajamii, waandishi wa habari na wanaharakati mbalimbali wa kidini na kimaadili wamekuwa wakiupinga sana muziki wa Bongo Fleva na kuuhusisha na maneno ya kihuni, tabia na mavazi yasiyofaa, matumizi ya dawa za kulevya, pombe, utovu wa

[2] Baraza la Sanaa la Taifa

maadili, upotoshaji jamii, mashairi yenye lugha ya ufyosi na athari za utamaduni wa kigeni. Maelezo ya wataalamu hao yanaashiria kwamba muziki wa Bongo Fleva unakengeusha misingi ya jamii na kuchagiza mmomonyoko wa maadili hususani kwa vijana, jambo linalochangia vikundi mbalimbali vya kijamii kuupinga muziki huo na hivyo kuonekana kuwa haufai.

Pelluro (2007) na Tupokigwe (2010) wanaitambua nafasi ya Bongo Fleva kama utambulisho muhimu wa vijana ambao huunganishwa na lugha maalumu kupitia uimbaji. Wanaeleza kuwa Bongo Fleva ni aina ya muziki unaopendwa sana na vijana. Tupokigwe (2010) anaongeza kuwa kuna ukengeushi mwingi wa kimaadili katika nyimbo hizi. Ukengeushi huo unajitokeza katika namna mbili, yaani lugha inavyotumiwa na wasanii wa Bongo Fleva na namna lugha hiyo inavyotafsiriwa na wanajamii. Hivyo, anashauri kuwa taasisi zinazojihusisha na masuala ya lugha na utamaduni nchini Tanzania zisipoangalia suala la utumizi wa lugha katika muziki wa kizazi kipya, hapo baadaye muziki huu utasababisha vijana kuwa na lugha yao. Maelezo ya Tupokigwe yanadhihirisha kuwa wasanii wa Bongo Fleva wanatumia lugha isiyofaa na inayokengeusha maadili ya jamii. Aidha, jamii pia inatoa tafsiri ya ziada ya maneno yanayoimbwa na wasanii ikiwa ni pamoja na kuyahusianisha na mchakato wa ngono. Jambo hili linachochea taasisi na asasi mbalimbali za kijamii kuupinga muziki huo na kuona kama chombo kinachopotosha jamii. Lugha inayotumiwa na wasanii wa Bongo Fleva ni jambo mojawapo lililochochea kufanyika kwa utafiti huu.

Usuli huo unaonesha kwamba tafiti nyingi zilizofanyika kuhusu nyimbo za Bongo Fleva hazijalenga kuchunguza dhima za matumizi ya ungonoshaji katika nyimbo hizo bali zimetazama lugha na maudhui yanayopatikana katika nyimbo hizo kama njia mojawapo inayopotosha jamii na kuua maadili ya jamii husika. Hali hiyo imesababisha baadhi ya nyimbo za Bongo Fleva kufungiwa, kwa mfano, wimbo wa Roma Mkatoliki (Ibrahim Mussa) na Stamina (Boniventure Kabogo) waliomshirikisha Maua Sama (Maua Salehe Sama) unaoitwa "Kibamia". Wimbo huo ulitoka Novemba 2017 na kupigwa marufuku Desemba 2017. Mwanzoni mwa mwaka 2018 wimbo huo ulifungiwa na BASATA kwa madai kwamba msanii ametumia lugha ya matusi ambayo ni kinyume na maadili ya Kitanzania.

Vilevile, wimbo wa "Mwanza" maarufu kama 'Nyege Nyegezi' ulioimbwa na Rayvany (Raymond Mwakyusa) akimshirikisha Daimond Platnumz (Nasibu Abdul Juma), ulifungiwa na BASATA Novemba 2018 hivyo haikuruhusiwa wimbo huo kusikika katika redio na runinga yoyote nchini Tanzania. Pia, wasanii hao walifungiwa kufanya matamasha yoyote ndani na nje ya Tanzania. Aidha, BASATA walieleza kuwa kitendo cha kuzifungia nyimbo hizo kinatokana na wasanii husika kuimba nyimbo zenye maudhui yanayohamasisha ngono, kutumia lugha ya matusi na isiyofaa, kuonesha dharau, utovu wa nidhamu na uvunjifu wa maadili uliokithiri (BBC Swahili, 2018). Sambamba na hilo, wimbo mwingine uliofungiwa ni "Kwangwaru" ulioimbwa na Harmonize (Rajab Abdul Kahali) akimshirikisha Daimond Platnumz. Wimbo huo ulipigwa marufuku na Bodi ya Kusimamia Filamu

nchini Kenya mwezi Machi 2019. Taarifa ya katibu mtendaji wa bodi hiyo ilieleza kwamba wimbo wa "Kwangwaru" hautaruhusiwa kupigwa, kuchezwa wala kuimbwa na wanafunzi katika shule zote nchini Kenya kwa sababu una ujumbe mchafu kuhusu mahaba (Mobeyo, 2018). Wimbo mwingine wa Bongo Fleva uliofungiwa na BASATA mwaka 2019 ni "Hallelujah" ulioimbwa na Diamond Platnumz na Morgan Heritage pamoja na wimbo wa "Wakawaka" ulioimbwa na Diamond Platnumz. Aidha, katika kufafanua sababu za kufungiwa kwa nyimbo hizo katibu mtendaji wa BASATA akinukuliwa na gazeti la Mwananchi la Agosti, 2019 anaeleza kuwa "BASATA inazidi kufungia nyimbo zote zinazoendelea kuchezwa licha ya kutokuwa na maadili. Tumeshawakanya wasanii wetu vya kutosha na tumesisitiza wazingatie maadili yetu. Nyimbo hizi na zingine nyingi zinazokiuka maadili na kutumia lugha isiyoifaa tutazidi kuzifungia". Sababu za nyimbo za Bongo Fleva kufungiwa zinaelezwa na Simiyu (2020) kuwa wanamuziki wa Bongo Fleva wana mazoea ya kukaidi sheria zinazoelekeza juu ya maadili na uhusiano wa kijamii kwa kutumia lugha inayoashiria ungonoshaji katika kazi zao, jambo linalotazamwa kama ni kinyume na maadili ya jamii. Maelezo haya yanaonesha kuwa nyimbo nyingi hufungiwa kutokana na ukiukwaji wa maadili.

Maelezo ya wataalamu na hatua zinazochukuliwa na mamlaka husika zinazohusiana na tasnia ya sanaa, vinaonesha wazi kuwa jamii inapinga vikali matumizi ya lugha inayoashiria ungonoshaji na kwamba ni upotoshaji na ukiukaji wa maadili na misingi ya jamii za Kiafrika. Ukiukaji huo umejengwa katika hoja kwamba baadhi ya jamii za Kiafrika hulitazama suala la ngono kuwa ni siri na masuala yote yanayolihusu ikiwa ni pamoja na mafunzo hupaswa kufanyika katika hali isiyokuwa ya wazi (Ayisi, 1962; Van Pelt, 1971; Karama, 2019; Wanjala, 2020). Maelezo haya yanabainisha kuwa jamii inalitazama kwa mtazamo hasi suala la lugha inayotumika katika Bongo Fleva hasa matumizi ya lugha ya ungonoshaji na kwamba husababisha mmomonyoko wa maadili (Karama, 2019). Kutokana na mtazamo huo, katika makala hii tumechunguza matumizi ya lugha ya ungonoshaji katika ushairi wa Bongo Fleva huku mifano ikitolewa kutoka wimbo wa "Kwangwaru" wa Harmonize na Diamond Platinumz (2018) pamoja na wimbo wa "Baikoko"[3] wa Mbosso na Daimond Platnumz (2020).

[3] Baikoko ni aina ya uchezaji wa ngoma inayopatikana pwani ya Afrika ya Mashariki hususani katika maeneo ya Tanga na Mombasa.Baikoko ni ngoma ya asili ambayo miondoko na uchezaji wake huhusisha utendaji unaohusianisha ishara za matendo ya ngono (Jegame, 2017). Pia, ngoma hii inaitwa Baikoko kutokana na aina yake ya uchezaji ambapo wanawake hucheza na kuonesha madoido mbalimbali kwa kuzungusha sehemu yao ya makalio pamoja na kuchezesha mapaja yao kwa haraka kulingana na mdundo wa muziki. Ngoma hii huruhusu wanenguaji hao kumwagiwa maji nyuma ya makalio yao wakiwa wanacheza huku wakiwa wamevalia nguo laini na zinazoonesha maumbile yao kwa uwazi kama vile kanga (Urban Dictionary.com, 2017). Baikoko ni utamaduni asilia wa Wadigo wa Tanga ambapo wanenguaji hucheza muziki asilia wa chakacha na ngoma zile zenye asili ya mkoa ya mkoa huo. Aidha, ngoma hii ilianza kutambulika mapema katika miaka ya 1990 (Buule, 2023).

## 2.0 Methodolojia ya Utafiti

Data za makala hii zilipatikana kwenye akaunti ya *YouTube*. Sampuli iliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa ambapo mtafiti alisikiliza nyimbo mbalimbali akilenga zenye matumizi ya maneno yanayoashiria mchakato wa ngono ambazo zimesikilizwa na kutazamwa na watu wengi katika akaunti hizo. Pia, usampulishaji ulizingatia kwamba watunzi wa nyimbo teule wana haiba ya kuimba nyimbo zinazohusisha masuala ya ngono kwa kiasi kikubwa, hivyo, kuweza kutosheleza data za utafiti. Kwa mujibu wa Mrikaria (2007) na Mnenuka (2010), uwasilishaji wa kazi za fasihi na muziki ukiwamo pamoja na ufafanuzi wa lugha ya picha kama matumizi ya ishara na taswira mbalimbali vimerahisishwa sana kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kwa msingi huo, mbinu ya ukusanyaji data iliyotumika ni usikilizaji makini na utazamaji wa video. Mtafiti alitumia matini zenye sauti na picha mnato kisha kuhusisha nyenzo mbalimbali kama maleba, udhihiti wa sauti, vitendo na miondoko ilivyotumika katika utendaji na uwasilishaji wa nyimbo hizo. Mbinu hii ilisaidia kubaini matumizi ya lugha yanayoashiria ngono. Kufanikisha uchambuzi huo, Nadharia ya Moduli Anuwai ilimsaidia mtafiti kufanya uchambuzi wa nyimbo teule na kubainisha dhima za matumizi ya lugha ya ungonoshaji katika nyimbo hizo teule.

## 3.0 Nadharia ya Moduli Anuwai

Nadharia ya Moduli Anuwai iliasisiwa na Gunther Kress (2001) na Theo van Leenwen (2010). Nadharia hii inajikita kuchunguza namna maana inavyoweza kuzalishwa na kuwasilishwa kupitia muunganiko wa moduli mbalimbali zaidi ya kuwapo kwa matumizi ya lugha. Matumizi ya moduli hizo ndiyo huchochea uelewa wa wasikilizaji wa kazi husika. Moduli hizo huonesha lugha ilivyotumika, picha zilivyoundwa, muonekano wa kimaudhui na maana iliyotengenezwa. Hivyo, matini moja hubeba maana kadhaa kutokana na namna mitindo mbalimbali ya lugha, picha na maudhui yanayowasilishwa hasa katika kipindi hiki cha kidijiti. Nadharia ya Moduli Anuwai hupambanua mawasiliano kwa namna mbalimbali kama kusikia, kuona, kuhisi, matini andishi, matendo na mijongeo ya mwili pamoja na njia zingine za kisemiotiki kama matumizi ya kiishara na taswira. Kupitia moduli hizo ndipo maana ya ujumbe uliowasilishwa hupatikana. Aidha, waasisi wa nadharia hii wanabainisha kuwa mawasiliano ni moduli anuwai ya kurithi ambayo huhusisha uelewa wa namna moduli anuwai zingine tofauti zinavyoingiliana, zinavyohusishana na kufanikisha ufasili wa maana. Waasisi wa nadharia hii wanaeleza kuwa matini yoyote inapounganisha mifumo ya kisemiotiki miwili au zaidi hutafsiriwa kuwa ni moduli anuwai. Hivyo, ili mawasiliano yanayofanyika yaeleweke, ni lazima yahusishe muunganiko wa mifumo mbalimbali ambayo huwapo kwa lengo la kusaidia kupatikana kwa maana ya kile kinachowasilishwa. Mifumo hiyo hutambulika kama moduli ambazo huweza kuwa ni lugha, matamshi, ishara, picha, utendaji, maleba, muziki, miondoko na mijongeo mbalimbali. Moduli hizo ndizo

hufanya kazi ya kuunda maana na kumwezesha msikilizaji, mtazamaji na msomaji kufasili maana husika ya kinachowasilishwa.

Nadharia ya Moduli Anuwai huhusisha dhana tatu muhimu. Mosi, ni mitindo anuwai; hizi ni hazina za kijamii na kitamaduni zinazounda na kuzalisha maana kama vile lugha, picha, ishara na sauti. Pili, ni mkusanyiko wa moduli mbalimbali; huu ni muunganiko wa moduli anuwai tofauti zinazofanya kazi pamoja kuunganisha maana. Tatu, ni mahusiano ya ndani ya kisemiotiki. Hii ni namna moduli tofauti zinavyoingiliana na kuchochea kila moja kuunda na kuzalisha maana. Nadharia ya Moduli Anuwai imejengwa katika mihimili mikuu mitatu. Mhimili wa kwanza ni uchanganuzi wa kimuktadha wa mfumokazi wa moduli anuwai. Huu ni mhimili unaotazama ni kwa namna gani lugha na moduli zingine zinatumika kuunda maana katika muktadha wa kijamii. Mhimili huu umetusaidia kufungamanisha muktadha wa matumizi na matumizi ya lugha yaliyotumika katika nyimbo teule. Mhimili wa pili ni uchanganuzi wa moduli anuwai ya semiotiki ya kijamii. Huchunguza namna maana inavyotengenezwa kupitia mifumo ya kijamii na miingiliano ya kitamaduni. Mhimili huu umetusaidia kufafanua maana za ishara, taswira na alama mbalimbali na namna zinavyorejelea mambo fulani kwa kuzingatia tamaduni husika. Mhimili wa tatu ni uchanganuzi wa moduli anuwai katika mkusanyiko wa maandishi. Mhimili huu huhusisha kiwango kikubwa cha seti za data kutoka katika matini za moduli anuwai ili kubainisha namna moduli mbalimbali kama lugha, maandishi, sauti, ishara na picha zinavyotumika na kuunda maana ya kinachowasilishwa. Hii inamaanisha kwamba nadharia hii imejikita kutazama mitindo mbalimbali iliyotumika katika uwasilishaji wa kazi husika na namna mitindo hiyo inavyotengeneza na kuzalisha maana. Mhimili huu umesaidia kupata maana kwa kuunganisha moduli zote kama lugha, ishara za kisemiotiki, sauti, picha na maandishi.

Hivyo, misingi yote mitatu ya nadharia hii imesaidia kuchambua dhima za matumizi ya lugha ya ungonoshaji katika ushairi wa Bongo Fleva. Nadharia ya Moduli Anuwai imekuwa faafu kwa sababu imesaidia kubaini mitindo anuwai, mathalani, matumizi ya lugha kama taswira, taashira na tafsida pamoja na matumizi ya sauti na utendaji ulivyotumika katika nyimbo husika. Mitindo hiyo anuwai ndiyo imetusaidia kuelewa namna lugha ilivyotumika katika nyimbo husika na kuweza kufasili maana ya kilichowasilishwa. Hivyo, maana zilizotolewa ni muunganiko wa moduli anuwai mbalimbali kama vile lugha, sauti, taswira na taashira pamoja na utendaji vilivyojitokeza katika nyimbo teule. Nadharia hii imeteuliwa kwa sababu inahusisha muunganiko wa mitindo mbalimbali ya kidijiti ambayo inajitokeza katika uwasilishaji wa muziki wa Bongo Fleva.

## 4.0 Matumizi ya Lugha ya Ungonoshaji katika Muziki wa Bongo Fleva

Katika sehemu hii dhima za matumizi ya ungonoshaji katika muziki wa Bongo Fleva zimejadiliwa. Uchambuzi umeongozwa na misingi ya Nadharia ya Moduli Anuwai. Nadharia hiyo imetusaidia kubainisha na kufafanua dhima za matumizi ya ungonoshaji katikaushairi wa Bongo Fleva.

Kabla ya kuwasilisha matokeo ya utafiti, ni vyema kutoa muhtasari wa nyimbo teule ili kujenga msingi mzuri wa ufafanuzi wa matokeo ya utafiti. Katika kutoa muhtasari wa nyimbo hizo, makala imeanza na wimbo wa "Kwangwaru" kisha wimbo wa "Baikoko" umefuata. "Kwangwaru" ni wimbo ulioimbwa wa sanii wawili ambao ni Harmonize na Daimond Platnumz. Wimbo huu umekitwa katika kumsifia mwanamke na kuonesha namna anavyopaswa kuwa mbunifu, mwajibikaji na fundi anapokuwa kitandani. Msanii anaeleza namna alivyomsaliti mwanamke wake wa zamani kutokana na kushindwa kumridhisha wanapokuwa faragha. Hivyo, anamdokeza mwanamke wake mpya kuwa anapaswa kuwa mjuzi na mbunifu kitandani ili asiweze kusalitiwa. Kwa upande wa wimbo wa "Baikoko", umeimbwa na wasanii wawili ambao ni Mbosso na Diamond Platnumz. Wimbo huu unahusu sifa mbalimbali anazopewa mwanamke ambaye katika wimbo huu anarejelewa kama mwali. Huyu ni mwanamke aliyezaliwa na wazazi wanaotoka katika makabila yenye tamaduni za kuwafunda watoto wa kike, yaani masuala ya unyago, hivyo, kumjengea ujuzi na ubunifu wa kuhimili na kumiliki kitanda. Msanii anatoa sifa za umbo, ufundi wa mapenzi na sifa za unenguaji za mwali. Sifa zote zinazotajwa ndizo zinawafanya wasanii watamani kumwona akicheza baikoko, ambayo ni ngoma maarufu ya kabila la Wadigo mkoani Tanga.

### 4.1 Dhima ya Mawasiliano

Imebainika kuwa matumizi ya lugha ya ungonoshaji katika muziki wa Bongo Fleva huwa na lengo la kufanikisha mawasiliano. Matumizi ya lugha ya ungonoshaji katika muziki wa Bongo Fleva hufanyika kimkakati kwa lengo la kuwasilisha mawazo, imani na matamanio waliyonayo juu ya maisha hususani masuala yanayohusu ngono. Kwa mfano, katika Data Na. 1 ya ubeti wa kwanza wa wimbo wa "Kwangwaru" msanii anasema:

(1)
*I wish ningekuwaga na mavumba,*
*Mkwanja na manoti*
*Nikuhonge vya thamani...,*
*Ama, niwe fundi wa kuigiza ka' Kanumba*
*Masanja, Joti usiwe mbali nami...*

*...usiwaamini ukishawapa wanakwenda..."*
*Oh, basi jilegeze*
*Nikubebe mgongoni ! iyelewi*
*Deka nikudekeze nikutunze kama mboni! (iyelewi)*
*wakija wapoteze jifanye kama huwaoni! (iyelewi)*
*Kisha uniongeze ulivyofunzwa unyagoni...(iyelewi).*

**Chanzo:** "Kwangwaru" (Harmonize na Diamond Platnumz, 2018)

Data Na. 1 inaonesha namna msanii anavyowasilisha mawazo yake juu ya umuhimu na nafasi ya pesa katika mahusiano ya kimapenzi. Pia, anasisitiza umakini hasa katika suala la kuweka imani juu ya mtu unayempenda. Msanii anataja baadhi ya mifano ya waigizaji kama Kanumba, Masanja na Joti. Lengo la msanii si kueleza kuwa waigizaji hawana mapenzi ya kweli, bali ni kufikisha maudhui kwamba kuna mapenzi ya kweli na ambayo siyo ya kweli, yaani yaliyojaa maigizo. Pia, anadokeza nafasi ya ufundi na ubunifu wa kimahaba katika mahusiano. Katika kiitikio msanii anasema: "deka nikudekeze nikutunze kama mboni, wakija wapotezee jifanye kama huwaoni, kisha uniongeze uliyofunzwa unyagoni". Kwa kuzingatia moduli anuwai ya kisemiotiki tumebaini kuwa msanii anatumia taswira 'mboni' kuashiria hali ya thamani anayompa mwenza wake. Msanii anawasilisha matamanio yake na kuonesha namna anavyoweza kumthamini na kumtunza mwenza wake kama mboni ya jicho. Pia, msanii anatumia taswira 'unyagoni' kurejelea mafunzo maalumu wanayofundishwa wanawake juu ubunifu na mbinu mbalimbali kuhusu masuala ya unyumba. Msanii amezingatia matumizi ya lugha katika kuwasilisha mawazo na matamanio yake ya kingono. Hivyo, ni dhahiri kuwa matumizi ya lugha ya ungonoshaji yana dhima ya kufanikisha mawasiliano.

Sambamba na hilo, msanii anaonesha umuhimu wa mawasiliano baina ya wapenzi juu ya namna wanavyoweza kuridhishana kimahaba. Msanii anaamini kuwa mawasiliano hayo humpatia nafasi kila mmoja ya kuwa wazi na kueleza hisia zake juu ya mambo anayopenda kufanyiwa na mwenza wake wanapokuwa faragha. Haya yanajitokeza katika Data Na. 2 ya ubeti wa kwanza wa wimbo wa "Kwangwaru" anaposema:

(2)
*...ungependa juu au chini kwenye uvungu wa uparemiwa,*
*Nikumbatie baridini kwenye tundu kama njiwa.*
*Moyo wangu ni wa makuti usinijie na kiberiti, haya wee!*
*Penzi likageuka chuki nyumba ikawa kibiti,*
*Nipatie vya kitandani nipe hadi kwenye kiti,*
*Ili asiniingie shetani nawe nikaja kukuchiti...*

**Chanzo:** "Kwangwaru" (Harmonize na Diamond Platnumz, 2018)

Katika nukuu hii msanii ametumia matumizi ya lugha kama taashira za kingonoshaji kuwasilisha matamanio yake ya kingono. Kwa mfano, ametumia taashira ya ungonoshaji 'uvungu wa uparemiwa' kuashiria sehemu ya haja kubwa. Msanii anamuuliza mwenza wake kuwa angependa matumizi ya uke au njia ya haja kubwa. Kuwapo kwa swali hili kunaashira nia ovu na ukengeufu wa jamii juu ya matumizi ya sehemu asilia katika mchakato wa ngono. Pia, kuna matumizi ya taashira 'tundu' ambayo imetumika kuashiria uke ilhali 'njiwa' imetumika kuashiria uume. Pia, anasema kuwa "ungependa juu au chini kwenye uvungu wa uparewima" akionesha kuwa suala la unyumba linahitaji mawasiliano na ushirikiano baina ya mwanamume na mwanamke. Taashira hizo ni mojawapo ya moduli anuwai za kisemiotiki. Moduli

hizo ndizo zimejengwa na namna lugha ilivyotumika kufinyanga maudhui yaliyokusudiwa. Ufafanuzi wa matumizi ya lugha umefanyika kwa kuzingatia mhimili wa pili wa Nadharia ya Moduli Anuwai unaojikita kuchanganua moduli anuwai ya semiotiki ya kijamii ambapo tumeangalia maana ilivyotengeneza na namna inavyofungamana na utamaduni wa jamii. Katika nukuu hiyo, tunaona matumizi ya lugha ya ungonoshaji yanatumika kama njia ya kulipiza kisasi. Msanii Diamond anakejeli na kuonesha udhaifu wa mwanamke wake wa zamani kwamba hakuweza kumtosheleza wakiwa kitandani. Kutokana na udhaifu huo anamwomba mke wake wa sasa atumie ufundi alioupata unyagoni, ubunifu, vionjo na mitindo tofauti ili amridhishe kimapenzi. Vilevile, anamtahadharisha kuwa kushindwa kumridhisha na kumpa unyumba kwa namna ambayo ataridhika kutasababisha amsaliti na aende kwa wanawake wa nje. Matumizi ya lugha ya ungonoshaji yametumika kama njia ya kufanikisha mawasiliano.

Vilevile, msanii ametumia taswira za ungonoshaji kufanikisha mawasiliano. Tazama Data Na. 3 ambayo ni kiitikio cha wimbo wa “Kwangwaru” kama ifuatavyo:

(3)
*Oh, basi jilegeze*
*Nikubebe mgongoni (iyelewi)*
*Kitandani nikoleze*
*Kwa miuno ya Kingoni (iyelewi)*
*Kisha nibembeleze*
*Nirudishe utotoni (iyelewi)*
*Weka mate niteleze*
*Kama nyoka pangoni (iyelewi)*

**Chanzo:** “Kwangwaru” (Harmonize na Diamond Platnumz, 2018)

Katika Data Na. 2 msanii anaanza kujenga fikra za ungonoshaji kwa hadhira yake anaposema, “oh basi jilegeze, nikubebe mgongoni”. Haya ni matumizi ya moduli anuwai ya kisemiotiki ambayo msanii ametumia lugha ya picha na ishara kurejelea umuhimu wa kutengeneza mazingira ya utayari na maandalizi kwa ajili ya faragha. Msanii anamjengea hali mwenza wake ya kujihisi ana ujuzi na ubunifu wanapokuwa kitandani. Anamwaminisha kuwa mapenzi anayoyapata yana uwezo wa kumrudisha katika hali ya utoto. Baada ya matumizi ya moduli hiyo ya kisemiotiki msanii anatumia taswira za kingono anaposema, “weka mate niteleze kama nyoka pangoni”. Taswira ya ‘mate’ imetumika kuashiria kilainishi kinachopakwa ukeni. Pia, kuna taswira ‘nyoka’ iliyotumika kuashiria uume ilhali taswira ‘pango’ imetumika kuashiria uke. Mwimbaji anatumia kitenzi ‘teleza’ anapokinyumbua na kusema ateleze kama nyoka pangoni akiwa na maana mate yatumike kama kilainishi kinachomsaidia kuingiza uume wake ukeni pasi na shida yoyote wakati wa kufanya ngono. Matumizi ya taswira hizi yanadhihirisha kuwa matumizi ya lugha ya ungonoshaji katika muziki wa Bongo Fleva yana dhima ya mawasiliano. Msanii ametumia lugha ya ungonoshaji kuwasilisha matamanio yake kwa mwenza wake.

Matumizi ya lugha ya ungonoshaji yanajitokeza pia katika wimbo wa "Baikoko" na kudhihirisha kuwapo kwa dhima ya mawasiliano. Msanii anatumia lugha ya ungonoshaji kujenga fikra za tendo la ngono akilini mwa wasikilizaji. Haya yanajitokeza katika Data Na. 4 anaposema:

(4)
*Nyuma kalisasambua*
*Kafungasha midambwada (bwada)*
*Anavyotafuna muwa*
*Ka kibogoyo dada! (Woo!)*

**Chanzo:** "Baikoko" (Mbosso na Diamond Platnumz, 2020)

Katika Data Na. 4 msanii ametumia matumizi ya lugha ya picha kama "nyuma kalisasambua, kafungasha midambwada". Msanii anatumia moduli anuwai ya kisemiotiki ambayo inajipambanua kupitia msimbo wa kiishara kwa lengo la kurejelea maumbile ya mwenza wake. Baada ya msimbo huo, msanii anatumia taswira "anavyotafuna muwa". Msanii anajenga fikra za kingono kwa msikilizaji kupitia kitendo cha kutafuna muwa ambao ni mmea wenye shina refu na pingili nyingi kama mwanzi. Mmea huo husifika kwa utamu kutokana na kuwa na maji yenye sukari. Pia, ni mmea wenye ugumu katika kutafuna, hivyo, unahitaji kutumia nguvu ili kutoa maji yenye utamu ambayo mtumiaji huyafyonza. Msanii anatumia taswira hiyo kuashiria kuwa tendo la ngono lina ladha ya utamu na ili kuupata utamu huo wahusika wanahitaji kutumia utashi na nguvu. Pia, anatumia taswira hiyo kuashiria kuwa tendo la ngono hufanyika kupitia mdomo na mtendaji anapaswa kumung'unya uume mdomoni kama mtu asiye na meno ili asiweze kuuumiza. Kinachobainika ni kwamba katika data hiyo, matumizi ya lugha ya ungonoshaji yamelenga kutimiza azma ya mawasiliano baina ya wenza. Hii ina maana kuwa matumizi ya lugha ya ungonoshaji hulenga kukidhi haja ya mawasiliano.

Sambamba na hilo, matumizi ya lugha ya ungonoshaji yanajitokeza pia kupitia taswira na taashira kama inavyoonekana katika Data Na. 5 ya ubeti wa wimbo wa "Baikoko" kama ifuatavyo:

(5)
*Ye ni* ***sisimizi*** *na mimi* ***gegedu*** *tuna**gegeduana** (gegedu)*
*Nilivyo sina jinsi*
*Tajiri wa mbegu*
*Namhonga hata mwana...*

**Chanzo:** "Baikoko" (Mbosso na Diamond Platnumz, 2020)

Katika mshororo wa kwanza wa nukuu hii, msanii anatumia taswira ya 'sisimizi' ambaye ni mdudu mdogo mwenye umbo na sura kama siafu ilhali 'gegedu' ni mchwa mkubwa mwenye kichwa chekundu na sifa au tabia ya ukali. Matumizi ya taswira ya wadudu hawa yanapambanua umuhimu wa tofauti za kirika katika

mahusiano baina ya mwanamume na mwanamke. Hivyo, anaonesha kuwa yeye mwanamume ni mkubwa kuliko mwanamke. Moduli ya kisemiotiki imetusaidia kubaini kuwa sisimizi na gegedu vimetumika kiishara kuashiria tofauti za kimaumbile. Hivyo, katika muktadha wa wimbo huu matumizi ya lugha ya ungonoshaji yametumika kama njia ya kufanikisha mawasiliano baina ya wenza. Kwa mujibu wa BAKITA (2022), 'gegedua' ni kitendo cha kutafuna kitu kigumu kwa juujuu kama anavyofanya mbwa anapokula mfupa. 'Gegeduana' ni kitenzi ambacho kimenyambuliwa katika hali ya utendano {-an-}. Kinyambuo cha utendano hurejelea dhana ya kufanyiana tendo baina ya pande mbili. Katika upanuzi wa maana, imekuwa ni hali ya kawaida kujenga dhana ya tendo la ngono kupitia kauli ya kutendeana (Ngunguti na Mapunda, 2022). Kwa mfano, maneno kama 'kulana', 'kufanyana' na 'kutiana' hujenga taswira ya tendo la ngono kutokana na kuongezewa viambishi vya kutendeana. Hivyo, neno 'gegeduana' limetumika kujenga taswira ya tendo la ngono (Lukas, 2022). Hii ina maana kuwa matumizi ya lugha ya ungonoshaji hulenga kufanikisha uwasilishaji maudhui juu ya ubunifu na mitindo mbalimbali inayoweza kutumiwa wakati wa faragha.

Sambamba na hilo, imebainika kuwa vijana wengi wa Kitanzania ni wapenzi wa kusikiliza na kutazama video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya zenye maudhui ya ngono. Nyimbo zenye maudhui ya kingono zilizopo kwenye akaunti za *YouTube* za wasanii wa muziki wa kizazi kipya, zina watazamaji wengi zaidi. Kwa mfano, Agosti 2025 wimbo wa "Kwangwaru" ulikuwa umesikilizwa na watu milioni 130 ilhali "Baikoko" ulisikilizwa na watu milioni 66. Hivyo, ni dhahiri kuwa matumizi ya lugha ya ungonoshaji katika muziki wa Bongo Fleva yana dhima ya kufanikisha mawasiliano. Wasanii hutumia ungonoshaji kama njia ya kuwasilisha matamanio na maudhui ya kingono ili kupata nafasi ya kusikilizwa katika soko la muziki, kuivutia hadhira, kukidhi uhitaji wa jamii hususani elimu na matamanio yanayohusu masuala ya kingono. Jambo hilo linachochea wasanii kuzidi kupigia chapuo matumizi ya lugha ya ungonoshaji katika muziki wa Bongo Fleva.

### 4.2 Kubainisha Umuhimu wa Mafunzo ya Jando na Unyago

Imebainika kuwa dhima mojawapo ya matumizi ya ungonoshaji katika Bongo Fleva ni kubainisha umuhimu wa mafunzo ya jando na unyago katika jamii. Jando na unyago ni mojawapo ya asasi za kijadi zinazotoa mafunzo ya kijadi katika jamii kwa kuzingatia miiko ya jamii husika. Jando ni mafunzo anayopewa mtoto wa kiume kwa lengo la kumtoa kutoka katika hali ya utoto kwenda utu uzima ilhali unyago humhusisha mtoto wa kike. Kijana ambaye hakupitia jando na unyago hakuruhusiwa kuoa au kuolewa, kwani ni dharau kubwa kwa jamii (Rashid, 2013; Maondo, 2017). Mafunzo ya jando na unyago ni muhimu kwa wanajamii na hutumika kama daraja la kumvusha kijana kutoka kwenye utoto kuelekea hatua ya utu uzima. Kutokana na umuhimu huo, wasanii wa Bongo Fleva hutumia ungonoshaji kama mbinu ya kuieleza jamii umuhimu wa kuendeleza utoaji wa mafunzo ya jando na unyago kwa

vijana. Haya yanajitokeza katika Data Na. 6 ambayo ni mishororo ya wimbo wa "Kwangwaru" kama ifuatavyo:

(6)
*...Wakija wapoteze jifanye kama huwaoni, Iyelewi,*
*Kisha uniongeze* ***ulivyofunzwa unyagoni...***
*… Kitandani nikoleze kwa* ***miuno ya Kingoni…***

**Chanzo:** "Kwangwaru" (Harmonize na Diamond Platnumz, 2018)

Katika Data Na. 6 msanii anaeleza kwamba anahitaji kufanyiwa kwa kadiri ya mafunzo ambayo mwenza wake alipatiwa akiwa unyagoni. Anaongeza kuwa anahitaji kukolezwa na viuno vya Kingoni. Msanii ametumia taswira "unyagoni" kurejelea mafunzo ya jadi kuhusu masuala ya unyumba wanayopewa wanawake. Pia, anataja "viuno vya Kingoni" akirejelea mitindo mbalimbali anayopaswa kufanyiwa wakati wa faragha. Hii inaonesha wazi kuwa mafunzo ya unyagoni yana nafasi kubwa katika masuala ya unyumba na uimarishaji wa ndoa. Rashid (2013) anaeleza kuwa mafunzo ya jando na unyago katika baadhi ya jamii za Kitanzania kama Wayao, Wamakonde na Wangoni ni muhimu kwa sababu humuandaa kijana kukabiliana na majukumu ya kiutu uzima ikiwa ni pamoja na masuala nyeti ya ndoa, yaani unyumba, uwajibikaji katika kuridhishana na kustareheshana. Anaongeza kuwa mabinti hupewa mafunzo kwa njia ya majaribio juu ya namna ya kumridhisha mume wakati wa kumpa chakula cha ndoa, usafi, uvumilivu, heshima na malezi ya familia. Hali hii inaakisi mafunzo aliyopewa binti kupitia "Utenzi wa Mwanakupona" kuwa ajitahidi kuwa na ubunifu katika kumpa mapenzi mwanamume hadi apumbazike (Mulokozi, 1999). Lengo la mafunzo hayo ni kuwafundisha vijana maadili mema, masuala ya ndoa, unyumba, malezi na uwajibikaji ilhali kwa upande wa binti hulenga kumjengea ubunifu, uimara, ustahimilivu na kuimarisha nyumba yake. Msanii anaonesha kuwa kukosekana kwa mafunzo hayo kunaondoa ubunifu ambao athari zake ni kushindwa kuridhishana kimapenzi. Haya yanajitokeza katika Data Na. 7 ambayo ni mishororo ya wimbo wa "Kwangwaru" kama ifuatavyo:

(7)
*…unataka kucheza* ***chura*** *na ungali umesimama, we inama inama*
*Asa waoneshe unachezaje,*
*Unataka* ***maji ya kisima****, na muoga kuchutama, we inama inama*
*Hebu waoneshe unachotaje, we inama inama*
*Unataka* ***kupiga deki****, wima umesimama, inama inama*
*Si unataka* ***vya pool table****, wima umesimama*
*Hebu tuoneshe unapigaje…*

**Chanzo:** "Kwangwaru" (Harmonize na Diamond Platnumz, 2018)

Data Na. 7 hapo juu inabainisha kuwa ili kutimiza hitaji la ndoa kuna mafunzo yanayohitajika hasa kumjengea mwanamke ujasiri na ubunifu katika kuimarisha

suala la unyumba. Msanii anatumia tafsida kama ‘kucheza chura na angali umesimama, unataka maji ya kisima na angali umesimama, unataka kupiga deki angali umesimama, unataka vya *pool-table* angali umesimama’. Msanii ametumia ishara kurejelea umbile la chura na miondoko yake. Umbile la chura huonesha namna mgongo wake ulivyo juu na miondoko yake ya kujitikisa anavyoruka. Msanii anatanabahisha namna mwanamke anavyopaswa kuinama na kucheza kimiondoko ya chura. Pia, msanii anadokeza kuwa katika hali ya kawaida huwezi kuchota maji kisimani ikiwa umesimama, ni lazima itakupasa uiname ndipo uyachote. Utashi na ufasaha wa ufanyaji kazi hizo umejengwa katika hali ya mtendaji kuinamisha kiwiliwili chake chini huku eneo la makalio yake likipaswa kuwa juu ili kukamilisha zoezi husika kwa ufanisi. Msanii ametoa mafunzo juu ya mitindo na mbinu zinazoweza kutumika kuimarisha utendekaji wa tendo la ngono kwa kutumia ulinganisho uliofumbatwa katika matumizi ya tafsida. Kinachobainika ni kwamba wasanii wanakutana na udhibiti wa kimaadili katika jamii, hivyo, kushindwa kuwasilisha mambo muhimu yanayohusu masuala ya unyumba. Kutokana na ugumu huo, wasanii huzingatia matumizi ya lugha ya ungonoshaji ili kukidhi haja ya wanajamii kwa kuelimisha masuala yanayohusu unyumba kwa njia ya burudani. Kwa mantiki hiyo, kuzifungia nyimbo zenye matumizi makubwa ya lugha ya ungonoshaji ni kupoteza vipaji na kuinyima jamii elimu. Hivyo, taasisi mbalimbali za kijamii na kisanaa zinazohusika na suala la maadili ni muhimu kutumia njia mbadala za kiteknolojia kama programu tumizi zenye nywila ambazo zitaruhusu hadhira lengwapekee kupata maudhui. Njia hii itasaidia kundi rika fulani kufikiwa na maudhui kusudiwa.

Aidha, suala la umuhimu wa utashi, weledi, ubunifu na madoido ya kimahaba linajitokeza pia katika wimbo wa “Baikoko” na kuonesha nafasi ya tashititi za kimahaba katika kufanikisha suala la unyumba. Msanii anaeleza kuwa starehe anayoipata kutoka kwa mwenza wake wakati wa tendo la ndoa ni namna anavyopinda mgongo akiinama na kuinuka huku akifuata uume ulipo. Anaongeza kuwa ‘kwa madoido na mbwembwe mwali anainama na kuisusa’ ili kumpatia uhuru mwenza wake kufaidi tendo la ndoa kwa kadiri anavyoweza. Haya yanajitokeza katika Data Na. 8 ambayo ni mishororo ya ubeti wa pili kama inavyoonekana hapa chini:

(8)
*Anainama anainuka mwali anaifuata*
*Kwa kujishebedua*
*Anainama anainuka mwali anaisusa*
*Anainama hataki mwana*
*Anainama anainuka mwali anaifuata*
*Kwa madoido*
*Anainama anainuka mwali anaifuata (Brra)*

**Chanzo:** “Baikoko” (Mbosso na Diamond Platnumz, 2020)

Nukuu hii inaonesha namna msanii anavyomsifia mwali wake juu ya uwezo, ubunifu na ujuzi wa mitindo mbalimbali aliyonao na namna anavyotumia ujuzi huo kumridhisha wanapokuwa faragha. Msanii anaongeza kwamba ujuzi wa kimahaba alionao mwanamke wake ni wa kurithi na ameupata kutoka kwa wazazi wake anaposema kuwa "baba Mndenge na mama Mzaramo, uno lake la kurithi, aaah". Msanii anadai kuwa licha ya kurithi, mtoto ni mahiri wa kimahaba kutokana na uwezo wake wa kukata viuno na kudaka magoli wakiwa faragha. Uwezo huo hujipambanua zaidi anavyokata viuno, kuutikisa uume huku akidaka magoli. Msanii anatumia moduli ya kisemiotiki kama taswira 'kipa' inayotumika kuashiria uwezo alionao mwenza wake wa kudaka magoli yanatoka kwa mchezaji ambaye ni mwanamume wanapokuwa uwanjani. Msanii anadokeza uwezo wa mwanamke wake wa kudaka magoli hayo huku akiwa anazungusha kiuno. Hayo yanajidhihirisha katika Data Na. 9 kama ifuatavyo:

(9)
*Eboh! mtoto anadaka*
*Golikipa Ronyamila (wabeja)*
*Tena akikata anaitikisa sababu (brr, okay)*

**Chanzo:** "Baikoko" (Mbosso na Diamond Platnumz, 2020)

Msanii ametumia moduli ya kisemiotiki kama matumizi ya lugha ya picha kuelezea utendaji kazi na ubunifu wa mwanamke wake wanapokuwa faragha. Matumizi ya lugha isiyo ya wazi yanatokana na kuwapo kwa udhibiti wa kimaadili ambao hauruhusu masuala ya ngono kuelezwa kwa uwazi kutokana na imani kwamba imani kwamba ni chanzo cha mmomonyoko wa maadili. Udhibiti huo hufifiza utoaji wa wazi wa elimu na mafunzo yanayohusu masuala ya ndoa. Aidha, Saidi (2009) anaeleza kuwa jando na unyago ni chanzo cha kuporomoka kwa maadili katika jamii, kushuka kwa kiwango cha elimu, mimba na ndoa za utotoni pamoja na magonjwa ya zinaa. Mtazamo wa Saidi (2009) unapingwa na Karugendo (2020) na Rashid (2013) wanapotazama jando na unyago kama suluhu ya changamoto za kimaadili zilizopo katika jamii zetu. Wanaeleza kuwa jando na unyago ilikuwa ndio 'chuo cha malezi' kilichotumika kuwakamilisha vijana kitabia, kimalezi, kiuwajibikaji na kuimarisha ndoa na familia zao. Vijana waliopita katika mafunzo hayo walikamilika kimaadili na kiutendaji. Hivyo, suala la utandawazi limeua mafunzo haya na kusababisha mmomonyoko wa maadili kwa wanajamii. Aidha, Karugendo (2020) anaongeza kuwa dini zimekuwa zikipiga vita utamaduni wa jando na unyago. Dini hizo za kigeni, zilileta utamaduni mpya na kuzika utamaduni wa Kiafrika bila kufanya utafiti wa kutosha ili kakuchuja kwa lengo la kuondoa mabaya na kuacha mazuri. Mtazamo huu unashikiliwa na viongozi wengi wa kidini ambapo wanasisitiza zaidi mafundisho ya dini yanayomjenga mwanajamii katika misingi ya dini zaidi na kusahau mahitaji muhimu ya mwanadamu kama kutoshelezwa kimapenzi. Kwa mtazamo huu, ni dhahiri kuwa kuzifungia nyimbo za Bongo Fleva zenye matumizi makubwa ya ungonoshaji si njia stahiki ya kukabiliana na mmomonyoko wa maadili. Hivyo, jamii

na asasi za kimaadili zinapaswa kutafuta njia mbadala itakayosaidia jamii kujifunza masuala ya unyumba kwa uwazi pasipo kuharibu maadili ya jamii.

### 4.2 Kuonesha Ubunifu wa Kiutunzi

Imebainika kuwa matumizi ya lugha ya ungonoshaji katika muziki wa Bongo Fleva hulenga kuonesha ubunifu wa kiutunzi. Muziki ni kazi ya fasihi ambayo inahitaji kuzingatia ubunifu katika namna ya upangiliaji wa mishororo, uteuzi wa maneno na matumizi ya lugha kwa upekee wake. Matumizi ya lugha ndiyo msingi unaopambanua ubunifu wa kifasihi ukitofautisha na mazungumzo ya kawaida yaliyozoeleka katika jamii. Mulokozi (2017) anaeleza kuwa nyimbo na mashairi vinaingiliana katika vigezo vya muhimu kama vile nudhumu, yaani utunzi wa kufuata kaida fulani za urari na kuteua maneno machache yanayowakilisha dhana pana. Sifa hii ya nudhumu hufanya utunzi wa nyimbo kuwa tofauti na kazi nyingine za sanaa. Pia, utunzi wa nyimbo huhusisha ubunifu mkubwa katika matumizi ya lugha kwa sababu ndiyo hubeba maana ya kilichowasilishwa kwa kuzingatia muktadha na utamaduni husika. Msanii huzingatia matumizi ya lugha kwa kuteua maneno na mbinu za kisanaa ambazo zitagusa hisia za hadhira, kujenga mahadhi ya wimbo na kuwasilisha ujumbe husika kwa wakati mmoja. Matumizi ya lugha ya ungonoshaji kama njia ya kuonesha ubunifu, yanajitokeza kuanzia mwanzo hadi mwisho wa wimbo wa “Kwangwaru” na “ Baikoko”. Kwa mfano, tazama Data Na. 10 ya mishororo ya wimbo wa “Kwangwaru” msanii anapoimba:

(10)
*Uniongeze ulivyofunzwa* ***unyagoni***
*Asa dance nikuone,* ***Kwangwaru***
*Wabamijo, Kwangwaru*
*Ululu feni, Kwangwaru...*
*...ungependa juu au chini kwenye* ***uvungu wa uparemiwa****,*
*Nikumbatie baridini kwenye* ***tundu*** *kama* ***njiwa****.*
*Moyo wangu ni wa makuti usinijie na kiberiti, haya wee!*
*Penzi likageuka chuki nyumba ikawa kibiti,*
*Nipatie vya* ***kitandani*** *nipe hadi kwenye* ***kiti****,*

**Chanzo:** “Kwangwaru” (Harmonize na Diamond Platnumz, 2018)

Data hii imejengwa na matumizi ya lugha kama taswira zinazoashiria ungonoshaji. Ufasili wa taswira hizo unaongozwa na mhimili wa Nadharia ya Moduli Anuwai ambao unazingatia uchanganuzi wa kimuktadha wa mfumokazi wa moduli anuwai. Kupitia mhimili huo tunaona namna lugha na moduli zingine zinatumika kuunda maana katika muktadha wa kijamii. Kwa mfano, katika Data Na. 10 kuna matumizi ya taswira ‘Kwangwaru’ inayoashiria kitendo cha kukwangua au kusugua. Pia, kuna matumizi ya taashira ‘kama uvungu wa uparemiwa’, ‘tundu’ ikiashiria uke na ‘njiwa’ ikiashiria uume. Vilevile, matumizi ya lugha mengine ni kama ‘kitandani’ na ‘kiti’ vikiashira mitindo mbalimbali ya ungonokaji. Matumizi ya lugha yaliyojitokeza

katika data hiyo yanaonesha ubunifu wa mtunzi katika kufinyaga lugha na kutumia mbinu za kisanaa kuwasilisha ujumbe kwa njia isiyo ya wazi. Matumizi ya lugha ya ungonoshaji yanaonesha ubunifu mkubwa wa watunzi wa muziki wa Bongo Fleva. Pia, yanaonesha namna wasanii wanavyotumia ubunifu wao kuzingatia suala la maadili ya jamii. Hii ni kwa sababu wangeweza kuimba masuala yanayohusu ngono kwa uwazi zaidi pasi kutumia lugha ya picha. Sambamba na hilo, matumizi ya lugha ya ungonoshaji na dhima ya ubunifu wa kiutunzi yanajitokeza katika wimbo wa “Baikoko”. Tazama Data Na. 11 ifuatayo:

(11)
*Ye **sisimizi** na mimi **gegedu** tuna **gegeduana***
*Na nilivyo sina jinsi*
*Tajiri wa mbegu na mwonga hata mwana*
*Baba Mndenge mama Mzaramo*
*Uno lake la kurithi aaah*
*Kafunga tenge, mwana chakaramu shetani mwana ibilisi*

**Chanzo:** “Baikoko” (Mbosso na Diamond Platnumz, 2020)

Katika nukuu hii msanii anatumia taswira ‘sisimizi’ kuashiria mwanamke na ‘gegedu’ kuashiria mwanamume. Pia, anatumia ‘kugegeduana’ kuashiria utendekaji wa ngono. Matumizi ya lugha yanaonesha ukomavu wa kiubunifu wa mtunzi kwa sababu angeweza kutumia lugha ya kawaida kuwasilisha na kufikisha ujumbe wake kwa jamii. Lucas (2022) anaeleza kuwa utunzi wa nyimbo si jambo jepesi kutokana na kaida zake za kiutunzi, hivyo, ugumu wa kutunga nyimbo unaongezeka zaidi pale msanii anapotumia taswira za ungonoshaji. Msanii anahitaji ubunifu mkubwa wa kisanaa wa kuweza kubadilisha mazingira ya kawaida na kuyaleta katika muktadha wa ngono. Mtazamo huu unaonesha kuwa matumizi ya lugha ya ungonoshaji si kazi rahisi katika utunzi wa nyimbo za Bongo Fleva. Hivyo, msanii hutumia akili, utashi, maarifa na kuvifungamanisha na tamaduni pamoja na muktadha wa kingono ili kupata lugha inayoweza kubeba maudhui ya kingono aliyoyakusudia. Aidha, imebainika kuwa matumizi ya lugha ya ungonoshaji hupambanua ubunifu wa mtunzi kwa sababu msanii huwasilisha masuala ya ngono huku akipaswa kuzingatia maadili na miiko ya jamii. Hali hii inatokana na namna msanii anavyopaswa kutumia ubunifu wake kufinyanga masuala yanayohusu ngono kwa kutumia lugha ya picha, taswira, taashira na tafsida kwa kiasi kikubwa. Aidha, msanii hutumia ubunifu mkubwa kwa kuifinyanga lugha na kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa ili kukwepa udhibiti uliopo katika jamii unaojengwa na mtazamo kwamba masuala yanayohusu ngono yanapaswa kuwasilishwa kwa namna ya siri. Kwa mantiki hiyo, matumizi ya lugha ya ungonoshaji hayapaswi kuchukuliwa katika mtazamo hasi bali kama njia stahiki ya kuelimisha, kuburudisha, kuonesha ubunifu na kuwasilisha mawazo, matamanio na ujumbe ulioshindwa kuwasilishwa kwa njia ya kawaida kwa jamii.

**5.0 Hitimisho**

Matumizi ya lugha ya ungonoshaji katika ushairi wa Bongo Fleva hulenga kuwasilisha matamanio, shauku na hamu za kingono ambazo zimeshindwa kuwasilishwa kwa njia ya wazi kutokana na udhibiti wa kimaadili uliopo katika jamii. Matumizi ya lugha ya ungonoshaji hutumika kwa ustadi na hujipambanua kupitia kuwapo kwa mbinu zingine za kisanaa kama matumizi ya taashira, taswira na tafsida. Matumizi hayo yana dhima ya mawasiliano. Hii ina maana kwamba yanalenga kufanikisha mawasiliano baina ya msanii na jamii. Hutumika kuelimisha jamii umuhimu wa mafunzo ya jando na unyago na hupambanua ubunifu wa kiutunzi. Kutokana na sababu hizo tumebaini kuwa kuzuiliwa kwa nyimbo za Bongo Fleva zenye matumizi makubwa ya lugha ya ungonoshaji si njia stahiki ya kukabiliana na mmomonyoko wa kimaadili hasa katika zama hizi za kidijiti. Hivyo, BASATA na asasi nyingine muhimu zinazofungamana na masuala ya maadili ya wasanii na jamii, zinapaswa kutumia njia mbadala za kidijiti kama kuwa na programu maalumu zinazoweza kutumiwa kuruhusu nyimbo hizo kusikilizwa na rika na mazingira fulani ya watu. Programu hizo zina uwezo wa kuruhusu maudhui yanayohusisha ungonoshaji kuwekewa vigezo maalumu na nywila ambazo mwanajamii hawezi kutazama wala kusikiliza pasi kufuata taratibu. Jambo hili huweza kufanyika kama ilivyo katika maudhui ya kingono mengine ambayo yamezuiliwa mitandaoni na wanajamii hawawezi kuyapata kiurahisi. Hii ni njia mbadala ya kuruhusu maarifa, maudhui na mafunzo muhimu yaliyopo katika nyimbo hizo kuifikia hadhira husika.

**Marejeleo**


Ayisi, E.O. (1972) *An Introduction to the Study of African Culture*. Nairobi: East African Educational Publishers.

BAKITA (2022) *Kamusi Kuu ya Kiswahili*: Longhorn Publishers (T) Ltd.

Bamgbose, O. (2001) "*Legal and Cultural Approaches to Sexual Matters in Africa: The Cry of the Adolescent Girl*". *MIA Int'l & Comp*., Juz. 127: 127-144.

BBC Swahili (2018) "Kibao kipya cha nyota Rayvanny na Diamond Platumz chafungiwa na Basata" Inapatikana https://share.googles/XdrleEJi4WMjV5CG6. Ilisomwa terehe 20 Agosti 2025.

Brown, L.B. (2015) "What's in a name? Examining the creation and use of sexual orientation and gender identity labels". *Issues in Religious and Psychotherapy*, 37(1): 23-32.

Bulaya, J. (2010) "Bongo Fleva na Siasa: Uchambuzi wa *Ndiyo Mzee* na *Siyo Mzee* za Profesa J". *Mulika*, Juz. 29/30: 45-54.

Buule, G. (2023) "Baikoko: Suggestive dance that typifies Nyege festivals" Imepatikanahttp://www.monitor.co.ug/uganda/lifestyle/entertainment/baikoko-suggestive-dance-that-typifies-nyege-festival-4430220. Ilisomwa 27 Agosti 2025.

Chachage, C.S.L. (2002) *Ndani ya Bongo: Utandawazi na Migogoro ya Utamaduni*. Paper Presented at the Tenth Conference on the Political Environment in Tanzania, tarehe 17 Septemba 2002, Dar es Salaam.

Da Costa, A.L.G. (2016) *Semantic Change in William Shakespeare: A Case Study from Sonnet 130.* Tasnifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Leon, Buleria Unileon.

Deignan, A. (2016) From Linguistics to Conceptual Metaphors. Katika E. Semino na Z. Demjen (Wah.) *The Routledge Handbook of Metaphors and Languag*e. Oxfordshire: Routledge. kur. 62-83.

Edwarsd, T. (2016) *Men in the Mirror: Men Fashion, Masculinity, and Customer Society.* London: Bloomsburry Publishing.

Fourtson, IV, B.W. (2003) "An Approach to Semantic Change". Katika B.D. Joseph na R.D. Janda (Wah.). *The Handbook of Historical Linguistics.* New York: Wiley. kur. 64-81.

Freud, S. (1912) *An Outline of Psychoanalysis.* London: Penguin.

Goodness, D. (2024) "Kiswahili Community Speakers' Language Choice in Communicating Sexuality Issues", *Cogent Arts & Humanities,* Juz.11(1): 1-14, Inapatikana katika https://doi.org/10.1080/23311983.2024.2404303. Ilisomwa tarehe 22/07/2025.

Jackbson, R. (1980) *Language Relation to Other Communication Style*. Columbus: Slavica. Publishers.

Jegame, T. M. (2017) *Influence of Inigeneous Attitudes on Secondary Eduction as an Investment*: A case of Tanga District.Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria.

Jilala, H. (2016) "Muziki wa Hip Hop na Haki za Kijamii: Dhima, Changamoto na Mapendekezo". Huria Journal of the Open University of Tanzania, Juz. 21 (hakuna kurasa).

Kadallah, R.T. (2010/2011) "Muziki wa Bongo Fleva na Changamoto za Kimaadili katika Jamii". *Mulika*, Juz. 29/30: 94-99.

Karama, M. (2019) "Darasa la Kimaharajani za Nyakanga-Kungwi-Sheikh Juma Amiri kuhusu Unyumba". *East African Journal of Swahili Studies*, Juz. 4(1): 129-141.

Karugendo, P. (2020) "William Mkufya, Mwandishi wa *Ua la Faraja* na *Zirai na Zilani*". Karugendo Blog: News and Writing from Privatus Karugendo. Inapatikana katika http://www.karugendo.net/2010/03/william-mkufya.html. Ilisomwa tarehe 30 Machi 2025.

Kasiga, G. (2023) "Tathmini ya Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya Karne ya 21 Nchini Tanzania: Tija na Madhara yake". *Mulika*, Juz. 42(1): 66-82.

Kress, G. (2001) *Multimodality: A Social Semiotic Approach to Contemporary Comminication*. New York: Routledge.

Lucas, B.C. (2022) "Usawiri wa Taswira za Ngono katika Nyimbo za Bongo Fleva". *Jarida la CHALUFAKITA*, Juz. 4: 65-79.

Lupokela, A.P. na Msuya, M.B. (2010/2011) "Dhima ya Bongo Fleva katika Maadili na Malezi ya Jamii". *Mulika*, Juz. 29/30: 38-43.

Mahenge, E. (2010/2011) "Chimbuko la Muziki wa Hiphop ni Uasi au Sanaa za Maonyesho". *Mulika*, Juz. 29/30: 38-43.

Manyama, C. (2014) "Maana Ibuzi kwa Wazungumzaji wa Kiswahili Zama za Utandawazi (Maana za Ungonoishaji)". Manyamacharles.blogspot.com. Inapatikana katika http://manyama.net/2023/23/maana-ibuzi.html. Imesomwa tarehe 23 Oktoba 2023.

Maondo, P. (2017) "Pata Kujua Maana ya Unyago na Siri za Unyago". Inapatikana katika http://maondo.wordpress.com/2017/12maana-unyago.html. Imesoma tarehe 10 Januari 2024.

Mnenuka, A. (2010/2011) "Taswira ya Mwanamke katika Muziki wa Bongo Fleva. Mifano kutoka Nyimbo Teule". *Mulika*, Juz. 29/30, 69-87.

Mobeyo, S. (2018) "Kwangwaru ya Harmonize na Diamond Platnumz yafungiwa Kenya" Inapatikana https://share.google/JCbpztYErl02Tosa. Ilisomwa 20 Julai 2025.

Mrikaria, S. (2007) "Fasihi na Teknolojia Mpya". *Swahili Forum*, Juz. 14: 197-206.

Mturo, N.G. (2018) *Jiniuchawi na Ushirikina kama Mkakati wa Uchimuzi katika Riwaya Teule za Maundu Mwingizi.* Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Mulokozi, M.M. (1999) *Tenzi Tatu za Kale.* Dar es Salaam: TUKI.

Newman, J. (2015) *Semantic Shift. The Routledge Handbook of Semantics.* Oxfordshire: Routledge.

Ngunguti, M. na Mapunda, G. (2021) "Tafakuri ya Upolisemia na Usitiari wa Ungonoshaji wa Maneno katika Kiswahili cha Mazungumzo". *Mwanga wa Lugha*, Juz. 6 (2), 139-150.

Echi, S.O. (2018) "The Indigenous Concept of Sexuality in African Tradition and Globalization". *Global Journal of Reproductive Medicine,* Juz. 6(1): 1-5.

Omar, S. (2009) *Tanzania Hip Hop Poetry as Popul'ar Literature.* Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Perrullo, A. (2007) 'Here's a Little Something Local': An Early History of Hip Hop in Dar es Salaam, Tanzania 1984-1997. Dar es Salaam. The History of an Emerging East African Metropolis. British Institute and Mkuki na Nyota. Kur. 250-272.

Matić U. (2024) "Sexuality in Ancient Egypt: Pleasures, Desires, Norms, and Representations". *The Cambridge World History of Sexualities*, Juz. 2: 22-42.

Rashid, H.U. (2013) *Mafunzo ya Nyimbo za Jando na Unyago katika Jamii ya Wahyao wa Masasi, Tarafa ya Lulindi.* Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Richard, C. (2010) "The Pleasures of Revenge". *Journal of Mind and Behavior*. 31(4):196.

Rogers, K. (2011) *The Reproductive System*. New York. Britannica Educational Publishing.

Samwel, M. (2012) "Bongo Fleva Inapotosha Jamii": Je, ni Dai Jipya katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili?" Makala katika Mtandao wa Google Scholar ilisomwa tarehe 23 Agosti 2019.

______ (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: MEVELI Book Publishers.

Simiyu, W.F. (2020) "Uchi kama Mkakati wa Kulipiza Kisasi katika Muziki wa Kizazi Kipya: Mfano wa Wimbo wa "Kwangwaru" wa Harmonize na Daimond Platnumz". *Kiswahili*, Juz. 83:(1): 15-26.

Suriano, M. (2011) "Hip-Hop and Bongo Flavour Music in Contemporary Tanzania: Youths' Experiences, Agency, Aspirations and Contradictions". *Council for The Development of Social Science Research in Africa* , Juz. 3: 113–126.

Traugott, E.C. (2006) Semantic Change: Bleaching Strengthening Narrowing, Extension. Katika K. Brown (Mh.) *Encyclopidia of Language and Linguistics* (Toleo la 2) kur. 124-131.

Tupokigwe, A. (2010) *Nafasi ya Muziki wa Kizazi Kipya katika Lugha ya Kiswahili*. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania.

Van Leeuwen, T. (2010) *Multimodality in The Handbook of Discourse Analysis.* New York: Routledge.

Van Pelt, P. (1971) *Bantu Customs in Mainland Tanzania*. Tabora: T.M.P Book Department. Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publishers Ltd.

http://swahillab.blogspot.com/2016/04/baikoko-dance-from-tanga-tanzania.html?m=1

http://www.urbandictionary.com

http://youtu.be/0Wbc5ZwkAMw?si=ImIZOXGaNeHhZMDO

http://youtu.be/hGqzvbZnyQ?siBwLbcrrllRu_gCx2

http://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/makala/wanawake-na-mafunzo -unyago-2810706